

FOMU YA MKATABA WA UJENZI

A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA

1	MWAJIRI	Mkuu wa Chuo, Chuo cha Ualimu Singachini, S.L.P 586, Kny: Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia
2	JINA NA ANWANI YA FUNDI (Mwajiriwa)	Jina: SHUKURU MALEO Anwani: S.L.P 80771 - MOSHI Simu: 0764511926
3	ENEO LA UJENZI	CHUO CHA UALIMU SINGACHINI
4	MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI	KUJENGA NA KUKAMILISHA UJENZI WA MADARASA MATATU (3) NA OFISI MOJA.
5	GHARAMA YA UFUNDI (+ Skills Development Levy 4.5% of work service):	10,899,000/=
6	MUDA WA MKATABA (Tangu Kusainiwa kwa Mkataba):	Tarehe ya Kusaini. 31/01/2022 Muda: Tarehe ya Kuanza Kazi. Tarehe ya Kumaliza Kazi.
7	MASHARTI YA MALIPO:	<ul style="list-style-type: none"> • Hakuna Malipo ya Awali • Fundi atalipwa kwa awamu baada ya kazi husika kukamilika na kukaguliwa

B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kulingana na maelekezo ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Mwajiri atatoa vitendea kazi vyote kama "concrete mixer", toroli, karai, ndoo, chepe, ngazi, n.k.
3. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.
4. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
5. Fundi atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.
6. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asijiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.
7. Fundi atahusika na vitendo (*kama wizi, uharibifu wa mali za chuo*) vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.
8. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.
9. Ni marufuku Fundi au mafundi kuja kazini akiwa ametumia aina yoyote ya madawa ya kulevya, unywaji wa pombe na kuvuta bangi eneo la chuo. Ikibainika atachukuliwa hatua.
10. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Mitatu baada ya kazi kukamilika (*Retention Money*) na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.
11. Kiasi cha asilimia 4.5% kitakatwa na kuwasilishwa mamlaka ya mapato Tanzania (T.R.A) ikiwa ni kwa ajili ya SDL. (*Skills Development Levy 4.5% of work service*)
12. Ucheleweshaji wa Kazi:
 - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.
13. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:
 - Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri (*kutokana na fedha au vifaa*), Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kazi.

14. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi kupigana au kuonesha viashiria vya aina yoyote ya kuhatarisha kuvunja amani katika eneo la kazi.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanachuo na hatua kali zitachukuliwa.

MWAJIRI:

Saini:

Jina : CORNELIUS L. GASPER

SIMU: 0754973720

Cheo: MKUU WA CHUO

Tarehe: 31/01/2022

SHAHIDI WA MWAJIRI

Saini:

Jina: ANDERSON A. TOWO

SIMU: 0713838317

Cheo:MSHAURI ELEKEZI

Tarehe: 31/01/2022

FUNDI:

Saini:

Jina: SHUKURU MALEO

SIMU: 0764511926

Cheo:FUNDI MKUU

Tarehe: 31/01/2022

SHAHIDI WA FUNDI

Saini:

Jina: PETER L. MINJA

SIMU: 0658210248

Cheo: FUNDI MKUU MSAIDIZI

Tarehe: 31/01/2022

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU
SINGACHINI
P. O. Box 586-MOSHI